KULEA KIZAZI CHA KESHO KWA AJILI YA MAISHA YA KANISA.

Sehemu ya Kwanza

Maono Na Umuhimu Wa Kizazi Cha Kesho Katika Urudisho Wa Bwana.

Maandiko:Luka 18:16-17;Matendo 26:13-19;Hesabu 14:29-31.

I.Lazima tuone uthamana wa Kizazi cha Kesho na thamani yake mikononi mwa Bwana-Luka 18:16-17.

A.Iwapo kwa kweli tunataka kufanya kazi ya vijana,na kuifanya kwa njia ya uzito,tunafaa kumruhusu Mungu atufungue Macho ili tuweze kuona uthamana wa vijana na umuhimu w a o Mikononi Mwake;Tukiliona jambo hili,basi ,tutathamini hii kazi,na papo hapo tutakua n a moyo ndani mwetu kwa ajili ya hiyo kazi.:

1.Mtu yeyote anayemtumikia Mungu ni lazima awe na maono-Mith29:18;Matendo 26:13-19.

2.Maono kuu katika Biblia,ni Kwamba Mungu wa Utatu anataka kujimimina mwenyewe ndani mwa watu wake aliowachakua na kuwakomboa ili kuloesha utu wao kwa utatu wa uungu ilikuzalisha na kuujenga Mwili wa Kristo ambao kiishio chake ni Yerusalemu mpya-Waef4:4-6;Ufunuo 21:2,9-10.

B.Wakati wowote Mungu anapotaka kubadilisha enzi, au mabadiliko katika enzi fulani,ni lazima apate chombo cha kutumia;Lazima wote tuwe vyombo vyenye uthamana ili Bwana atutumie hizi siku za mwisho kubadilisha enzi hii-Ufunuo12:5-11,1:20;Dan 12:3;10:11,19.

C.Kazi ya Mungu ya kubadilisha enzi moja hadi nyingine hutekelezwa na wanadamu;Kabla ya enzi mpya kuanza,kila wkati kuna watu katika enzi inayopita ambao Mungu anawatumia kubadilisha enzi;Katika kila kazi ya Mungu ya kubadilisha enzi,Mungu hutumia vijana:

1.Kwa kuwa watu ambao Mungu hutumia kwa wakati fulani hatimaye hujikuta katika mwanguko,na kukosa kufilikia Lengo la Mungu,Mungu hulazimika kugeuza enzi,kuwa na mwanzo mpya ili kutekeleza kile ambacho anataka kukitekeleza katika enzi mpya.

2.Ile kazi ambayo Mungu anaifanya kwa wakati huu ni kumaliza enzi hii na kuleta enzi ya ufalme;lazima apate vyombo vya thamana;Hili ndilo Mungu anataka kufanya leo hii.

II.Kuenea na kusambaa kwa urudisho wa Bwana siku za usoni, kwa jumla inategemea kizazi kinakokuja;Bwana anahitaji watoto na vijana kwa ajili ya siku zijazo za urudisho wake.

A.Tunaweza kusema kwa hakika ya kwamba yeyote anayetumiwa na Mungu kuanzisha kitu kipya au yeyote ambaye amechaguliwa na Bwana kugeuza enzi,alikua ni kijana;ukiliona jambo hili utathamini vijana mbele za Bwana.

B.Isipokuwa Yoshua na Kalebu,wale waliyohitimu na waliyokuwa tayari kuimiliki nchi nzuri walikua ni vijana;walikua ni wale wa kizazi cha pili-Kumb1:35-36,11:2-7;Hesabu

14:29-31.

1.Kizazi cha pili hakikuyapitia mengi kama yale kile cha kwanza kiliyoyapitia lakini kilipata manufaa ya yale ambayo kizazi cha kuanza kilipitia.

2.Yale wazee walipitia yaliwajenga sana walio wachanga;kwa hivyo,Mungu angetayarisha urithi wenye utajiri na msingi imara kwa kizazi cha pili watu laki sita ambao walikua tayari na wamehitimu kuunda jeshi la kupigana pamoja Naye na kwa ajili Yake.

3.Tuko katika hali iyo hiyo katika urudishowa Bwana leo hii;mambo haya yanakabidhiwa walio wachanga katika urudisho wa Bwana na yatakuwa ya munufaa kwao kuwajenga na kuwatayarisha kupigana pamoja na Bwana na kwa ajili ya Bwana.

4.Iwapo mtu atawachwa pekee yake,atajikwaa kwa mda wa miaka kumi,lakini sasa kwa njia ya mwili,anaweza kujifunza mambo hayo hayo kwa jioni moja;iwapo ndugu kama huyo atachukua ushirika wa mwili,ataokoa wakati;matumizi ya mamlaka katika mwili ni kwa ajili ya kuyaondoa makosa,na kufupisha wakati.

C.Lazima kuwe na kikundi cha vijana ambao waameokoka,na wamepata msaada halisi wa kiroho leo hii,ili wapate uzoelefu wa kutosha na wamtumikie Mungu siku za usoni;iwapo hakuna vijana ambao Bwana anawapata leo hii,Tutakapoondoka hatutakua na mtu wa kuturithi;hivo kutakua na pengo.

D.Ukiliona jambo hili,utakua na mzigo moyoni kuwapenda vijana bila kujali iwapo ni wazuri au wabaya;hebu wandugu na wadada wampendao Bwana wawapende vijana kwa ajili ya siku za usoni za Kanisa na za urudisho.

III.Urudisho wa Bwana unasambaa kwa mwendo mzuri;iwapo kutakua na makanisa katika kila miji mikuu ya nchi zinazoongoza hapa duniani;iwapo miaka zijazo vijana wengi watakamilishwa,urudisho wa Bwana utasambaa kwa kasi:

A.Lazima tufuatilie na tukue katika maisha yetu ya kiroho,huku tukidumisha ushirika wetu na Bwana;tukijiweka wakfu kwa Bwana tukiwasiliana Naye katika mambo yote;Ili tuwe washindi wa Bwana ni Lazima tumpende Bwana na kutwaa kila nafasi tuliyo nayo Kumpenda-Matt 26:6-13.

B.Kizazi kipya kinafaaa kuvikwa na ukweli;wanahitaji kusoma Neno na Neno la Bwana lijae ndani mwao,na wao wenyewe waingia katika Neno ili wachangamane na Neno-Wakolosai 3:16,Zaburi 119:11.

C.Kizazi kipya kinafaa kujijenga na tabia nzuri.;wanahitaji kijizoesha katika tabia nzuri na maaadili mema ili wawe wa manufaa na kumtumkia Bwana.-Wafilipi 4:8,13

D. Kizazi kipya kinahitaji Masomo ya juu zaidi;vijana wetu wote ni lazima wasome wawe na shahada ya viuo vikuu,na wasome zaidi kuliko wale walio nje ya Bwana,wapate gredi za juu na waendelee mbele wapate shahada za juu zaidi katika masomo yao:

1.Pana haja kubwa ya vijana wenye masomo ya juu katika urudisho wa Bwana;Vijana nilazima wajitahidi wapate masomo bora.

2.Iwapo vijaana watatumia nguvu zao hivi,watakapofika miaka thelathini,wataweza kuanza huduma yao kama vile Bwana Yesu alivyofanya;wengi wakichukua njia hii,kamwe hatutakua na upungufu..